بسم الله الرحمن الرحيم

**Kwa Maongezi Matamu, Yenye Sumu kuhusu Mustakabali wa Lebanon na Kanda!**
**Mjumbe wa Marekani Tom Barrack yuko nchini Lebanon Kuimarisha Kukamilishwa kwa Makubaliano ya Amani na Uhalalishaji Mahusiano na Umbile la Kiyahudi!**
(Imetafsiriwa)

Mnamo Julai 7, 2025, katika mkutano na waandishi wa habari katika Kasri la Rais, Mjumbe wa Marekani Tom Barrack alitoa taarifa akisema kwamba **"Lebanon na kanda hii wana fursa nzuri ambayo lazima ichukuliwe,"** kwamba **"wakati umefika wa kubadilisha kanda hii,"** na kwamba **"kila mtu amechoshwa na kile kilichotokea,"** kama alivyoweka. Pia alisema kwamba **"usalama utavutia uwekezaji kwa Lebanon,"** kwamba **"Rais wa Marekani alithibitisha dhamira yake ya kuchangia kujenga amani na ustawi nchini Lebanon,"** na kwamba **"fursa inapatikana kwa Walebanoni kuifanya nchi yao kuwa Lulu ya Mashariki kwa mara nyingine tena."** Hata hivyo, mazungumzo haya matamu yamefunikwa na hitaji la kimsingi linalotafutwa na Amerika, lililoelezwa na Tom Barrack katika taarifa zake: **"Syria, ambayo haina kile Lebanon ilicho nacho, imetoka kwenye machafuko makubwa hadi kwenye matumaini,"** na **"imeanza mazungumzo na Israel, na kila mtu anaharakisha kufikia makubaliano!"**... Suala hilo likawa wazi mithili ya mchana: ni upanuzi wa ule unaoitwa “Mkataba wa Amani wa Abraham” kujumuisha Lebanon! Ama kuhusu matamshi ya afisi ya rais wa Lebanon kuhusiana na jibu kwa mjumbe wa Marekani, walieleza hili kama suluhisho la kina: "Rais wa Lebanon aliwasilisha mawazo ya Lebanon kwa ajili ya ufumbuzi wa kina kwa mjumbe wa Marekani," na kumfanya mjumbe wa Marekani kuelezea majibu kama "ya kuwajibika," na kwamba “jibu la Lebanon liko ndani ya wigo ambao Marekani inajaribu kufanikisha”! Je! Utawala wa Marekani unatafuta chochote isipokuwa kutia saini makubaliano ya amani kati ya Lebanon na umbile la Kiyahudi, kama ambavyo hivi sasa inajaribu kufanya kati ya Syria na umbile la Kiyahudi?! Je, utawala wa Marekani unatafuta chengine mbali na kuondoa madhihirisho yote ya nguvu nchini Lebanon na kwengineko, hata kama ni ya kiutendaji na tegemezi, ilhali inafanya kila iwezalo kwa kikosi chochote kitakacho zichukua kutimiza yale ambayo wapiganaji mashujaa waliyatimiza katika Kimbunga cha Al-Aqsa mnamo 7 Oktoba 2023, kwa vifaa na mahitaji machache?!... Upande muhimu zaidi wa harakati hii ambayo ni uvamizi wa kanda hii, na sio tu Lebanon, ni msimamo wa pamoja kati ya Marekani na umbile la Kiyahudi, katika umbo baya zaidi la uvamizi wa kikoloni, unaofupishwa kama "Mradi Mpya wa Mashariki ya Kati wa Amerika," na kuliwezesha umbile la Kiyahudi kucheza dori ya polisi ndani yake: Ni mradi mmoja wa kikoloni. Wana adui mmoja wa pamoja katika mradi huu, na umeelekezwa dhidi ya Umma wa Kiislamu kama Ummah mmoja.

Kwa Mayahudi na Amerika, kufuata mchakato wa kuhalalisha mahusiano na amani na Mayahudi kunahitaji mipango, ambayo muhimu zaidi ni kuondoa dhihirisho lolote la nguvu, hata tulivu, karibu na Mayahudi. Hii ni pamoja na silaha za Hizbullah, zikiwemo silaha za kambi za Wapalestina. Iwapo silaha hizi zingetumika ipasavyo usiku wa kuamkia tarehe 7 Oktoba 2023, au zingetumika hapo awali, bila ya kutegemea maamuzi ya kivitendo ya kisiasa ya Iran na maamuzi ya dola za kieneo, zingeleta tofauti isiyopingika, ya kimsingi, pengine hata kuhamasisha majeshi dhidi ya tawala zao... Hata hivyo, kinachoendelea nyuma ya pazia ni kinyume na kile kinachoonyeshwa na pande zote kwenye vyombo vya habari. Mjumbe huyo wa Marekani, kwa maneno ya kushangaza, aliielezea Hizbullah kuwa ni chama cha kisiasa, na kwamba kinachofanyika hakielekezwi dhidi yake kama chama cha kisiasa**: "Hizbollah ni chama cha kisiasa chenye kipengee cha kijeshi, na Hizbullah lazima itambue kwamba ina mustakbali na kwamba njia hii haijaelekezwa dhidi yake."** Waziri Mkuu Nawaf Salam alitangaza baada ya kukutana na mjumbe wa Marekani kwamba **"Hizbollah ni sehemu muhimu ya dola ya Lebanon!"** Hili linathibitishwa na kauli ya Naibu Spika wa Bunge la Lebanon Elias Bou Saab katika mahojiano yake na Al Arabiya mnamo Julai 6, 2025: **"Mazungumzo ya vyombo vya habari yanatofautiana na yale yanayotokea nyuma ya pazia, na maneno ya kutojali kwenye njia ya mazungumzo ni ya kawaida."** Hakika, matamshi ya Katibu Mkuu wa Hizbullah Naim Qassem katika hotuba yake wakati wa kumbukumbu ya Ashura katika vitongoji vya kusini mwa Beirut yanaonyesha mambo yanasimamiwa kwa siri. **"Upinzani ni mojawapo ya suluhisho..."** na kwa machaguo yanayopatikana, **"tuko tayari kwa amani ... kama vile tuko tayari kwa makabiliano na ulinzi,"** kuthibitisha umoja wa misimamo na mwelekeo wa pande zote, ambao unaendana na hamu ya Amerika ya amani na uhalalishaji mahusiano na umbile la Kiyahudi, licha ya kauli zote za moto na maneno ya watu wengi ambayo yanatangulia adui au mkutano wowote na wawakilishi wake! Imedhihirika pia kwamba Rais Joseph Aoun, ambaye kuridhika kwake kamili na Marekani kunadhihirika, anaongoza upande wa Lebanon kwenye njia hii ya kusalimu amri na kuhalalisha mahusiano kwa kuanza tena mawasiliano na Mayahudi kwa kuanza upya kuweka mpaka wa nchi kavu na usimamizi wake wa moja kwa moja wa uondoaji wa silaha za Hizbullah kutoka kusini na hata kaskazini mwa Mto Litani...

Kisha, kile kilichofichuliwa kama utangulizi wa kuhitimisha makubaliano ya kujisalimisha na kuhalalisha mahusiano na umbile la Kiyahudi, kwa kuamsha Kifungu cha 52 cha Katiba ya Lebanon, ambayo inatamka kwamba "Rais wa Jamhuri atafanya mazungumzo na kuhitimisha mikataba kwa makubaliano na Waziri Mkuu, na haitakuwa ya lazima isipokuwa baada ya idhini ya Baraza la Mawaziri. Mikataba pia itajulishwa Bunge pindi maslahi ya nchi na usalama wa serikali ukiwa unaruhusu hivyo," ikionyesha njia inayofuatwa na mamlaka za Lebanon kutoka juu kabisa! Ni njia ya kuelekea kufilisi kadhia ya Palestina na kumaliza hali ya uadui na Mayahudi!

**Waislamu wa Lebanon:** Tunasema wazi wazi: Kile ambacho serikali ya Lebanon inafanya, kutoka juu kabisa ya uongozi wake, kupitia vyombo vya kisiasa na vyombo vya habari vinavyokikuza, ni udhalilifu, uduni, uoga, fedheha, na kujisalimisha kwa umbile nyakuzi, vamizi ambalo husaliti maagano na makubaliano. Hayawezi kusifiwa chini hivyo kuhusiana na suala la kimsingi la Waislamu ambalo watu hawa wanataka kulitelekeza kwa visingizio hafifu, kama vile maazimio ya Mkutano wa Beirut, makubaliano ya Waarabu juu ya kujisalimisha, au kujisalimisha kwa mashirika ya Palestina wanayodai kuwa ndio wamiliki wa kadhia hiyo. Matokeo ya hayo yote ni kusainiwa kwa mikataba ya kikhiyana pamoja na Mayahudi kwa kisingizio cha maslahi ya kitaifa! Moja ya sifa kuu za sera ya Marekani katika kanda hii, ili kuhifadhi maslahi yake, ni kumakinishwa kwa umbile la Kiyahudi na kulifanya kuwa sehemu muhimu ya kanda hii. Watawala wa madhara, watawala wa Waarabu na Waislamu, wanakula njama nalo katika hili, ili uhaini ambao mwendazake Sadat alituhumiwa nao —na alikuwa mhaini— uwe sera ya umma ya watawala hawa!

**Enyi Waislamu wa Lebanon:** Fikra ya kulipokonya silaha umbile la Kiyahudi na kulipokonya silaha mikononi mwa Marekani na Mayahudi ni dhambi linalojulikana, kwa sababu nia ya asili ni kuendelea kupigana na Mayahudi na kuwadhuru. Jihad inaendelea, haswa katika kitovu cha Waislamu, ash-Sham. Salamah bin Nufayl amesema: “Ufunguzi ulipewa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), nikaenda kwake na kumwambia: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, farasi wamefunguliwa na silaha zao zimewekwa chini, vita vimeshusha mizigo yake, na wakasema: Hakuna kupigana.’ Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akasema:

«كَذَبُوا، الْآنَ جَاءَ الْقِتَالُ، الْآنَ جَاءَ الْقِتَالُ، إِنَّ اللهَ جَلَّ وَعَلَا يُزِيغُ قُلُوبَ أَقْوَامٍ يُقَاتِلُونَهُمْ وَيَرْزُقُهُمُ اللهُ مِنْهُمْ، حَتَّى يَأْتِيَ أَمْرُ اللهِ عَلَى ذَلِكَ، وَعُقْرُ دَارِ الْمُؤْمِنِينَ الشَّامُ»...

**“Wamesema uongo, sasa ndio vita vimekuja. Sasa ndio vita vimekuja. Hakika Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, Anazipotosha nyoyo za watu wanaopigana nao, na Mwenyezi Mungu Anawaruzuku kupitia wao, mpaka ifike amri ya Mwenyezi Mungu. Kitovu cha Waumini ni Ash-Sham.”**

Lakini silaha hizi (za Lebanon na Palestina) ambazo zilipoteza lengo lake na zilielekezwa kwenye nyoyo za ndugu zetu na familia nchini Lebanon na kwengineko, zilipotosha fahamu yenyewe ya silaha na chimbuko la matumizi na kubebwa kwake. Mpaka kuondolewa kwake kukawa ni hitaji la umma kwa jumla, bila kutofautisha kati ya ima zilielekezwa dhidi ya Mayahudi au Waislamu. Dhana hii ilitiwa nguvu na kuchochewa na kufeli kuzitumia silaha hizo kwa wakati ufaao na kwa namna iliyotakiwa usiku wa kuamkia tarehe 7 Oktoba 2023 na kuendelea, wakati wa matukio ya mabaya mno yaliyoikumba kanda hii!...

Pamoja na hayo yote, suluhisho pekee sahihi kwa umbile la Kiyahudi linabakia kuondolewa kwake kutoka katika ardhi ya Palestina, na kutoka katika kila sehemu ambapo mkono wake, uliolowa damu za Waislamu, umefika. Kuondolewa kwa nguvu.

Hata hivyo, kuondolewa huku kunaonekana kutowezekana bila ya kuwaondoa watawala wajinga wanaoizunguka Palestina, watawala wa madhara waliopandikizwa na kafiri, mkoloni Magharibi, wanaoendelea kuwatawala Waislamu! Hapa munaona jinsi watawala hawa wanavyozuia nusra yenu kwa watu wa heshima wa Gaza kwa nguvu na ukatili ili kuhifadhi viti vyao vya utawala. Wanafanya dhambi waziwazi kwa kuwasiliana na Mayahudi mbele ya macho yenu. Wanayazuia majeshi kuchukua hatua za kivitendo kuwanusuru wale wanaofanya kazi ya kusimamisha Khilafah ya Pili kwa kuzingatia mafundisho ya Mtume, ambayo yana dhamira ya kweli ya kupigana na Mayahudi! Netanyahu, akijua hatari ya hii, ameweza tu kuelezea hofu yake juu yake na kuibuka kwake kwenye mwambao wa Mediterania. Aliapa kuikabili na kuzuia kuibuka kwake popote pale. Na bila shaka itadhihiri, Mwenyezi Mungu akipenda, licha ya yeye na walinzi wake, watawala wasaliti, mikononi mwa waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu wanaoomba usiku na mchana kutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na bishara njema ya Mtume wake, rehema na amani ziwe juu yake.

Kwa kuhitimisha, wanayoyafanya watawala wa Lebanon na watawala wa kanda hii kwa jumla, na hasa ash-Sham, ni jambo la kulaumiwa, limeharamishwa na ni khiyana kwa Mwenyezi Mungu, Mtume wake na waumini. Ni wale tu wenye maslahi katika mambo yao wenyewe au mnafiki anayejipendekeza kwa tawala hizi ndio watapinga hili, wakiuza dini yao kwa pato la kidunia. Mwenyezi Mungu Mtukufu asema:

[وَلَا تُجَادِلْ عَنِ الَّذِينَ يَخْتَانُونَ أَنفُسَهُمْ إِنَّ اللهَ لَا يُحِبُّ مَن كَانَ خَوَّاناً أَثِيماً]

**“Wala usiwatetee wanao khini nafsi zao. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi aliye khaaini, mwenye dhambi.”** [An-Nisa 4:107]. Halipaswi kupita kwa kimya cha watu, watoaji maamuzi, na watu wenye mamlaka juu yake. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

«مَنْ رَأَى مِنْكُمْ مُنْكَرًا فَلْيُغَيِّرْهُ بِيَدِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِلِسَانِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِقَلْبِهِ، وَذَلِكَ أَضْعَفُ الْإِيمَانِ»

**“Yeyote miongoni mwenu anayeona jambo ovu, basi na alibadilishe kwa mkono wake, ikiwa hawezi basi kwa ulimi wake, ikiwa hawezi basi (achukie) kwa moyo wake, na hiyo ni Imani dhaifu zaidi.”**

**H.** 13 Muharram 1447
**M. :** Jumanne, 08 Julai 2025

**Hizb ut Tahrir**
**Wilayah ya Lebanon**